BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 21 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi Trilioni Tano, Bilioni Mia Moja Themanini na Mbili, Milioni Mia Nane Tisiini na Tano, Laki Moja Arobaini na Nne na Mia Nne na Mbili Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya tarehe thelathini Juni, Mwaka Elfu Mbili na Ishirini na Tano, kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo na Kuweka Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

125. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tarehe 23 Septemba 2021, Serikali ilizinduwa vitambulisho vya wajasiriamali kwa lengo la kuwasaidia kurasimisha shughuli zao, kuwatambua kisheria na kukuza mitaji yao.

(a) Je, ni kiwango gani cha vitambulisho hivi vimetolewa mpaka sasa kwa wajasiriamali katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

(b) Je, vitambulisho hivi hutolewa kwa gharama ya kiasi gani na kiasi gani cha fedha zilipatikana kwa kuuza vitambulisho hivi.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali kwa wajasiriamali ambao wamepata vitambulisho hivi.

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

239. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa bahati nzuri sana mila, silka na tamaduni mbali mbali za Wazanzibari zimeelezwa kwa kina kupitia vitabu na riwaya nyingi za zamani.

(a) Je, Wizara ina utaratibu gani wa kusaidia kupatikana machapisho mapya ya vitabu hivi ikiwemo Nyota ya Rehema na Kuli, kwa mantiki ya kuenzi utamaduni wetu.

(b) Kwa kiasi gani Wizara yako ikiwashirikisha waandishi nguli wa riwaya na tamthilia waliojizolea sifa nyingi kimataifa katika kuwainua na kuwarithisha waandishi chipukizi.

284. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ilianzisha 'Radio na TV Station' ambazo ni ZBC1 na ZBC2 zinazomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata taarifa sahihi na kwa wakati. Hata hivyo, yapo malalamiko kwamba ZBC2 ni chombo ambacho kilianzishwa na Shirika la Utangazaji lakini watendaji wa Shirika hilo, hawanufaiki nacho kwa lolote.

(a) Je, ni nani hasa mmiliki halali wa ZBC2 na Serikali inanufaika vipi na chombo hiki.

(b) Je, Serikali hupata mapato ya kiasi gani kupitia matangazo ambayo hurushwa kupitia chombo hiki cha ZBC2.

(c) Je, ni kwa nini wachambuzi wote wa ZBC2 si waajiriwa wa Shirika la Utangazaji la ZBC.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

95. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Kituo cha Afya Tungamaa kinakabiliwa na changamoto nyingi katika utoaji wa huduma zake kutokana na ukosefu wa madaktari na upungufu wa madawa. Na kwa kuwa kituo hicho ni muhimu kwa wananchi wa kijiji cha Tungamaa na Chuo cha Mafunzo cha Tungamaa. Na kwa kuwa changamoto hii imesababisha wagonjwa wengi kutafuta huduma za awali katika Hospitali ya Kinyasini, ambayo iko mbali na eneo hilo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha kituo hiki kwa kupeleka madaktari na kutoa madawa.

(b) Kuna tetesi za uwezekano wa kuhama kwa kituo hiki, Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa kijiji na Chuo cha Mafunzo wanaotegemea huduma za matibabu katika eneo hilo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha uwazi na ushirikishwaji wa jamii katika mchakato wa maamuzi kuhusu hatma ya Kituo cha Afya Tungamaa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi Trilioni Tano, Bilioni Mia Moja Themanini na Mbili, Milioni Mia Nane Tisiini na Tano, Laki Moja Arobaini na Nne na Mia Nne na Mbili Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya tarehe thelathini Juni, Mwaka Elfu Mbili na Ishirini na Tano, kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo na Kuweka Mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**21 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**